# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2024**

**DODOMA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule 0689821592**

**M/Mkuu wa Shule 0785203217**

**Matron 0710095012**

**Shule ya Sekondari ya**

**Wasichana Lucas Malia**

**S.L.P 11**

**10/06/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..........................................................................................**
**S.L.P………………………………………………………………………..**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA LUCAS MALIA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA MKOA WA LINDI MWAKA 2024**

2. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya .............

Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Lucas Malia ipo Mkoa wa Lindi Wilaya ya Ruangwa Kata ya Mnacho. Shule ipo umbali wa kilometa 1 kutoka barabara kuu ya Ruangwa-Nanganga.

Ukifika kijiji cha **Chimbila B**. Shule ipo upande wa kulia ukitokea Nanganga na ipo kushoto ukitokea Ruangwa. Nauli ya kutoka barabarani hadi shuleni ni shilingi elfu moja (1,000) kwa pikipiki.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **1/07/2024** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **30/06/2024** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **14/07/2024**

1. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**1.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni sketi za blue iliokolea (**Dark blue).** Sketi ziwe ndefu kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la sketi zisizidi sm 18 au inch 7 na nusu. Upana wa mkanda au belt usizidi sm 5 au inch Moja na nusu, Mshono ni V ya mbele kama sare ya polisi .

ii. Shati (blauzi) nyeupe mbili (2) au zaidi mikono mirefu tetroni – Tomato na tai ndefu rangi ya sketi.

iii. Kwa wanafunzi wa Kiislamu: vazi la Msikitini

- Nusu kanzu
- Hijabu ya tetroni nyeupe/juba na sio mtandio, isiwe na urembo wowote. Pia isiwe na urembo wa lessi na ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

iv. Sare ya Michezo ni Jezi (bukta na t-shirt) zambarau na raba nyeusi.Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksi jozi mbili nyeupe za shule vi. Sweta ya dark blue mbili (2);

vi. Gauni la kazi za nje la kitambaa kizito (shamba dress) rangi ya kijivu mshono wa solo, kama anavaa hijabu ashone ya rangi kijivu.

vii. Tisheti (T-shirt) mbili (02) rangi ya damu ya mzee yenye kola (form six) nyeusi na nembo ya shule(Zinapatikana shuleni).

viii. Track Suit damu ya mzee isiyobana kwa ajili ya maandalizi ya jioni.

**1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari (counter book) quire three kumi (10)

ii. **Ream (A4)** Mbili (2) kwa mwaka, moja kila muhula.

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika. \

iv. Godoro 3x6.

v. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology; v. Scientific Calculator;

vi. Nguo za ndani za kutosha

vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)

viii. Mashuka Jozi 2(blue bahari), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 ya blue*;*

ix. Ndoo 3 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

x. Soft broom moja;

xi. Hard broom moja;

xii. Brash ndogo za kusugulia sink za choo;

xiii. mopa moja;

xiv. Fagio la chelewa moja kila muhula;

xv. Sabuni ya chooni lita 5;
xvi. Aje na vifuatavyo kulingana na tahasusi yake kwa ajili ya usafi
xvii. Aje na laboratory coat kwa wanafunzi wa sayansi.

- **HGL & CBG** - Kwanja na Jembe lenye mpini.
- **HKL & HGK** - Jembe lenye mpini na panga
- **PCB & PCM** - Panga na Reki
- **PMC$_s$ & HGF$_a$**- Mikasi ya kukatia maua

### 1.3 Michango mbalimbali

Mzazi au mlezi unapaswa kuchangia michango ifuatayo kupitia akaunti ya shule Na. **71110026279** jina la akaunti: **LUCAS MALIA GIRLS SEC SCHOOL-NMB**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation); iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule; vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa; viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
vii. Uvutaji wa sigara;
viii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
ix. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiii. Kudharau Bendera ya Taifa;
xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xv. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4 Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali; ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

ii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iii. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule :**

**Jina la Mkuu wa Shule GLADNESS H. MAKONGWA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule 0689821592
- Makamu Mkuu wa Shule 0785203217
- Mwandamizi Taaluma 0694339735
- Mwandamizi Malezi 0710321802.

## ORODHA YA VITABU

### CHEMISTRY

1.Advanced chemistry physical and industrial by P.Mathew(2006)

2.Essentials of physical chemistry by Arun Bahil,B.S Bahil &G.D Tuli (2012)

3.Organic Part A&B by A.Abdullah &M.H Nkunya

4.Inorganic Part A&B by J.S.Maro Guerman&M.Mikesewala(1989)

5.Physical chemistry by Ddungu&J.B.A.Mihigo(1998)

6.Advanced level Inorganic chemistry Part I&II by Tanzania Institute of Education(1995)

7.Organic chemistry an introduction by Jack E.Fernandez(1982)

8.Uderstsnding chemistry for A-Level students

9.Conceptual chemistry for class XII&XI by S.K Jaini (2011)

10.Advanced level chemistry,fourth edition by Ramsden(2000)

### GENERAL STUDIES

1.General studies for Advanced level certificate,Form six(6)by Richard R.F.Mbalase(2011)

2. General studies for Advanced level certificate,Form five(5)by Richard R.F.Mbalase(2011)

3.Contemporary approach for Advanced level " General studies Notes"Form 5&6 by Nyambari C.M

Nyangwine,Godfrey Rutta Nyangwine,Steven O. Maluka(New syllabus(2009)

### HISTORY

1.Major issues in African history by Tanzania institute of education

2.History of modern Europe by peacock

3.How Europe underdeveloped Africa by w. Rodney

4.History in focus ;modern world history by Ben Walsh

5.Matering advanced level history book two,by Kato,A(2011)

6. Matering advanced level history book one,by Kato,A(2012)

**KISWAHILI**

1.Kimbunga –H.Gora(taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili)(tuki),1994

2.Mapenzi Bora –S.Robert (mkuki na nyota)

3.Chungu Tamu-T.A MVUNGI (Tanzania Publishing house ),1985

4.Fungate ya uhuru –M.S Khatibu (macmillan and aidan)

5.Vuta N'kuvute –Shafi(mkuki na nyota 1999)

6.Kufikirika-S.Robert (mkuki na nyota 2003)

7.Mfadhili –Hussein Tawa (Methew &stationery 2007)

8.Usiku utakapokwisha-Mbunda Msokile 2007

9.Morani-E.Mbogo

10.Nguzo mama-P.Muhando

11.Kivuli kinaishi-

12.Kwenye ukingo wa Thim-E.Hussein

13.Kunga za fasihi na lugha –M.Msokile(1992)

14.Fasihi-F.E.M.K.Senkolo 1984

15.Kitangulizi cha tafsiri nadharia na mbinu-Mwansoko ,H.J.M. (1996)

16.Nadharia ya lugha kidato cha tano na sita Suluhaya ,M.C.(2010) silabsi mpya.

17.Nadharia ya fasihi(kipya) J.A masebo chapa ya tisa.-silabasi mpya.

**18. Kamusi kubwa TUKI**

**BIOLOGY**

1.Dissecting kit

2.New understsnding Biology for A-level student by Glenn&S.Toole(1999)

3.Systematic and classification by L.K Msaki(1993)

4.Biology,A functional Approach b M.B.V Roberts(1971)

5.Advanced Biology :Principle and application by C.J.Clegg&D.G.Mackean(2000)

6.Biological Science by Taylor ,etal(1997)

7.S.Chand's Bioloy for class XI&XII by P.S Verma &B.P.Pandey(2005) 8.Guide to dissection by H.G.Q Rowett(2005)

**ENGLISH**

1.Macmillan Education Ltd 2000,Encounters from Africa ,Macmillan

2.Ayi Kwei Amah,1996,The beautiful ones are not yet born,EAEP

3.Chinua Achebe ,1991,a man of the people,BAEP

4.Ndunguru 1999 ,Divine Providence,mkuki na nyota

5.Magala Nyago,1985,The Rape of the Pearl Macmillan

6.Namige Kayondo,1995 Vanishing shadows, Macmillan

7.Danny Sato,1983,His Excellency the head of state, Macmillan

8.David Omowale,2002,A season of welting ,EAEP

9.Francis Lubuga ,1990,Betrayer in the city,Heinemann

10.Ngugi wa Thiong'o,et al 1982,I will marry when I want,EAEP

11.Bukenya,1984,The Bride, EAEP

12.Okot Omitah 1991,Lwanda Magere Heinemann

13.Henrick Ibsen ,1974,An Enemy of the people,Eyre Matheuen

14.John Ruganda 2005,Black Mamba, EAEP

15.Charles Mloka,2002,The wonderful surgeon and other poems,mkuki na nyota

16.Tanzania Institute of Education ,1996,selected poems,Print pak(t)Limited.

17.The real English textbook for Advanced level ,Dr, Kadeghe Michael

18. **Dictionary kubwa oxford (English to English)**

**GEOGRAPHY**

1.Principles of physical geography by Monkhouse(2008)

2.Landforms in Africa by collinBuckle

3.Statistics simplified by N.A.Saleem

4.Map reading by Mac Master

5.Human and Economic Geography by C.Morgan (1982)

6.Map reading ,General publications Ltd –dsm by Durra,S.E.(2003)

7.Geography An intergrated Apprpoach ;Fourth edition by David Waugh(2009)

8.Practical Geography for AFRICA by John .M.Pritchard(1990)

9.R.B.Bunnet (2007)General Geography in diagrams.

**ADVANCED MATHEMATICS.**

1. Pure Mathematics 1&2 JK Backhouse.
2. Understanding Pure Mathematics AJ sadler.
3. Competence Based Advanced Mathematics P.L Mayombya.
4. Essentials for A-level Pure Mathematics. Telemu Majigwa

**KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA *TANO* KWA MWAKA 2023**

**Mimi** ................................................................. nakutaarifu kuwa nimepokea barua ya kuchaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Lucas Malia.
**NIMEKUBALI/NIMEKATAA** nafasi hii baada ya kusoma na kuelewa yaliyoandikwa katika fomu na barua ya kujiunga.
Ninaahidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu kuwa nikishafika shuleni, nitazingatia kanuni, sheria na taratibu zote za shule kwa kipindi chote cha mimi kuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Lucas Malia. Na nimeelewa kanuni na taratibu zote za shule na sitajihusisha na vitendo vya uvunjaji wa amani shuleni, kushiriki kufanya fujo, vurugu, migomo, kuvuta bangi na matumizi ya madawa ya kulevya pamoja na makosa ya jinai. Nitatumia juhudi na maarifa katika kujiendeleza kwa manufaa yangu na Taifa kwa ujumla.

**Jina la mwanafunzi** .......................................... **Sahihi** .................... **Tarehe** ......
**Jina la Mzazi/Mlezi** .................................... **Sahihi** .....................**Tarehe** ..........

**FOMU NAMBA 1.**

**To the Medical Officer**

.............................................................................................

.............................................................................................

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO ....................................................**

Please examine the above named pupil and give us the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school students.

1. Blood................................................................................................................ 2. Stool ...................................................................................................................
3. T.B. Test ..............................................................................................................
4. Syphilis Test .........................................................................................................
5. Urine Examination ................................................................................................
6. Eye Test ...............................................................................................................
7. Chest Test ............................................................................................................
8. Ears Test ..............................................................................................................
9. Spleen ..................................................................................................................
10. Abdomen ...............................................................................................................
11. Pregnancy..............................................................................................................

ANY ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairment, infection, family diseases etc.

...........................................................................................................................................

.........................................................................................................................................

I certify that, the above pupil is suitable/unsuitable for secondary school students. If unsuitable give reasons:

...........................................................................................................................................

..............................................................................................................

Name of **Medical Officer**: .................................................. Signature ........................... Date: ............................................. Official stamp ...................................

**FOMU NAMBA 2.**

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. Mkoa ................................................ Wilaya ..............................................
2. Tarafa .................................................. Kata ..............................................
3. Mtaa/Kijiji ..................................................
4. Jina la Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ..................................................Saini......................

   Tarehe.................................... Mhuri................................. Simu........................
5. Michezo anayopendelea

| Na. | Jina la Mchezo |
|---|---|
| 1. | |
| 2. | |
| 3. | |
| 4. | |
| 5. | |

9. Nafasi yoyote ya uongozi aliyowahi kushika

| Na. | Aina ya Uongozi | Shule | Mwaka |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |
| 4. | | | |
| 5. | | | |

Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli, pia nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi pamoja na kuwa na bidii ya masomo.

**NB**: Pamoja na fomu hizi ambatanisha na cheti chako cha kuzaliwa na nakala ya matokeo.

**Jina la Mwanafunzi ..........................................Sahihi ..................... Tarehe ...............**

**FOMU NAMBA 3.**

**TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi ..........................................................................
2. Kazi ..................................................................................
3. Anuani ...................................... Namba ya simu ....................................
4. Mkoa .............................. Wilaya ............................ Tarafa ................................
5. Kata ...................................Mtaa/Kijiji ...................................................

6. Anuani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo

| Na. | JINA | UHUSIANO | ANAPOISHI | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |

Mimi Mzazi/Mlezi wa ...................................................................... ninaahidi kushirikiana na walimu pamoja na watumishi wote wa Shule ya Sekondari Lucas Malia katika kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokuwa shuleni.

Nitaomba kujulishwa mara moja endapo mwanangu ameenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za shule. Pia nitakuwa tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makosa atakayofanya.

**Jina la Mzazi/Mlezi .................................Sahihi .....................Tarehe ....................**